

HALMASHAURI YA WILAYA YA LONGIDO



Barua zote zilandikwe kwa
Mkurugenzi Mtendaji
Halmashauri ya wilaya Longido
Simu No. 027 – 2539603/2

S.L.P 84
LONGIDO,
ARUSHA

11/11/2019

TANGAZO LA KUKAMATWA NGAMIA MIA MOJA NA KUMI NA MOJA (111) KATIKA WILAYA YA LONGIDO AMBAO MMILIKI WAKE HAJATAMBULIKA

Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Longido, anautangazia Umma kuwa, Uongozi wa Wilaya ya Longido ulikamata Ngamia waliokuwa wamehifadhiwa katika Kijiji cha Eworendeke- Kitongoji cha Skarda mnamo tarehe 8/11/2019, jumla ya ngamia waliokamatwa ni **mia moja na kumi na moja (111)** ambapo mpaka sasa mmiliki wake hajajitokeza.

Kwa tangazo hili uongozi wa Wilaya ya Longido unatoa siku saba (7) kwa mmiliki/wamiliki wa Ngamia hao kujitokeza haraka, wafike Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W), Halmashauri ya Wilaya ya Longido ndani ya Siku saba (7) toka tarehe ya tangazo hili.

Endapo hatajitokeza mmiliki/wamiliki wa Ngamia hao, taratibu za kisheria kuhusiana na mali zilizokamatwa zitafuatwa.

Tangazo hili limetolewa na,

JUMAA MHINA
MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA YA LONGIDO